<p>Note: A lease outlines the conditions for which some or all of a security deposit or pet deposit is returned in full or in part. Usually, the rented unit or property must be in the same condition it was in when the tenant moved in for deposits to be fully returned. If there is damage or loss, the housing provider can keep some or all of the deposit for repairs and replacement.</p>	<p>Angalisho: Kontra inaeleza wazi wakati na sababu malipo ya mwanzo ao ya wanyama italipwa yote ao nusu tu. Kwa kawaida, kama ukitaka malipo ya mwanzo irudishwe yote, ni lazima uache nyumba kama vile uliikuta wakati wa kuhamia ndani. Kama kuna kitu kiharibika, mwenye nyumba anaweza kuchukua nusu ya malipo ao yote kwa ajili ya kununua ao kutengeneza vitu.</p>
<p>Utilities</p>	<p>Umeme na vinginevyo</p>
<p>Sometimes, electric, gas, water, and other utility costs are covered in the monthly rent. However, they are often not. For example, water and trash removal are sometimes covered, but other services are not. The lease must clearly state who pays for which utilities.</p>	<p>Kuna wakati umeme, gaz, maji na malipo ya matumizi mengine inalipwa katika kodi ya kila mwezi. Lakini mara nyingi sivyo. Kwa mfano, maji na kutupa takataka yanaweza kulipiwa ndani, lakini vitu vingine hapana. Ni lazima kontra iseme wazi nani atalipa vitu gani.</p>
<p>Appliances</p>	<p>Vifaa vya nyumbani</p>
<p>The lease will list what appliances are included in the unit. Most rentals come with a refrigerator, stove, dishwasher, and microwave. For included appliances, the housing provider is responsible for maintenance and repair as long as the appliance was not misused. Be sure to understand how your appliances work to avoid misuse. Ask for the owner's manual(s) and get help reading and understanding them if needed. Follow manual instructions. If you, the tenant, add appliances, you are responsible for the repair and maintenance.</p>	<p>Kontra itaonyesha vifaa gani viko ndani ya nyumba. Nyumba nyingi zinakuja na frigo, jiko, mashini ya kusafisha masahani, na micro-onde. Kwa vifaa vyenye viko ndani ya malipo, mwenye nyumba ndiyo atatengenezesha kama kifaa kinaharibika na kama wewe haukukutumia vibaya. Ni lazima ujue namuna vifaa vyako vinatumika ili kuepuka matumizi mabaya. Omba vitabu vya matumizi na omba pia msaada wa kuvisoma na kuvielewa. Fuata maelezo ya matumizi. Ikiwa wewe mupangayi unaongeza vifaa ni wewe ndiyo utavitengenezesha vikiharibika.</p>



<p>Note: Washing machines and dryers may be in the apartment/house, but probably not. Many larger apartment buildings have coin- or debit card-operated laundry equipment. The cost per load is between \$1.50 and \$4.00. Or, you may be charged based on time. Usually, you pay with quarters. Some buildings have pay-via-mobile app options. If not, be sure to find out where the closest laundromat is and how to use the machines there.</p>	<p>Angalisho: Mashini za kufua nguo na kukausha zinaweza kuwa katika nyumba, lakini mara nyingi sivyo. Majengo mengi makubwa yana vifaa vya kufulia vinavyoendeshwa na pesa au carte ya banki. Malipo ya kila fungo ya nguo ni kati ya 1,50 \$ (dollar moja na nusu) na 4 \$ (dollars ine). Ao bei inaweza kufuatana na wakati wa kufua. Kwa kawaida, unalipa kwa pesa 0,25\$ (kichele robo ya dollar). Kuna majengo yanakubali kulipa kwa simu ya mukono. Kama jengo yako haina haya yote, tafuta mahali pa kufua nguo karibu na ujifunze kutumia mashini huko.</p>
<p>Renter Insurance</p>	<p>Assurance ya Mupangayi</p>
<p>Housing providers may require you to have renter's insurance. Typically, a lease agreement or addendum will state what insurance is required and what needs to be covered in the policy.</p> <p>How Does Renter's Insurance Work?</p>	<p>Mwenye nyumba anaweza kukulazimisha upate assurance ya Mupangayi. Kwa kawaida, kontra au ongezo ya kontra itasema kama assurance ni ya lazima, na pia vitu gani vitakuwa ndani ya assurance.</p> <p>Assurance ya Mupangayi inatumikaka aye?</p>
<p>Notice of Entry</p>	<p>Tangazo ya kuingia</p>
<p>Although many states have laws requiring housing providers to give prior notice to their tenants before entering a unit, there are no laws in some states. This part of the lease will tell you about the requirements regarding advance entry notice by the housing providers' staff, e.g., maintenance workers.</p>	<p>Majimbo mingi inalazimisha wenye nyumba kutoa tangazo kwa wapangayi mbele ya kuingia mu nyumba, lakini majimbo ingine haina sheria kama ile. Hii sehemu ya kontra inaeleza sharti ya mwenye nyumba au wafanyakazi wake kutoa tangazo kwa mupangayi mbele ya kuingia katika nyumba.</p>
<p><i>NOTE: There are exceptions when housing provider staff can enter your unit without notice, such as in cases of emergencies situations like fire, plumbing or electrical problems.</i></p>	<p>ANGALISHO: Mwenye nyumba au wafanyakazi wake wanaruhusiwa kuingia kwako bila kutoa tangazo mbele kukiwa hatari kama vile moto, au shida ya bomba au ya umeme.</p>
<p>Renewals</p>	<p>Kontra mupya</p>
<p>A renewal is when a housing provider gives you, the tenant, the option to extend your lease before it expires. Depending on the lease, some automatically renew for a year and others require you to state your intent to renew 30 to 60 days before the lease ends.</p>	<p>Mwenye nyumba anaweza kukuruhusu usiye kontra mupya mbele ya ile ya kwanza kumalizika. Kufuatana na kontra, mupya inaweza kuanza moja kwa moja kwa muda wa mwaka ingine moja. Kontra zingine zinalazimisha mupangayi aombe kontra mupya siku 30 au 60 mbele ya mwisho wa kontra ya kwanza.</p>
<p><i>NOTE: A housing provider is NOT required to extend or renew a lease and can change the terms and conditions, including the rent price, at renewal time.</i></p>	<p>ANGALISHO: Mwenye nyumba HALAZIMISHWI kuongeza au kuendeleza kontra ya kwanza. Wakati wa kusinye kontra mupya, anaweza kubadilisha tarehe za upangayi, sharti za kupangisha, na hata bei ya kupangisha.</p>
<p>Early Termination Fees</p>	<p>Malipo ya Kuhama Mapema</p>
<p>Leases include an early termination clause to protect housing providers if you, as a tenant, decide to break a lease</p>	<p>Katika kontra kuna sehemu inamulinda mwenye nyumba kama wewe mupangayi unaamua kuacha</p>



<p>before the termination date. The clause outlines the circumstances for a lease to be broken and cites fees due for breaking a lease early. These fees are usually one-to-two-months' rent, though some leases require full payment of the remainder of the lease. That is why you, as a tenant, need to remember that a lease is a contract and early termination has financial consequences.</p>	<p>nyumba mbele ya tarehe ya mwisho wa kontra. Hiyo sehemu inaeleza sababu za kuvunja kontra na bei ya kuvunja kontra mbele ya wakati. Kwa kawaida, bei ni mwezi moja au mwezi mbili ya kodi. Kuna kontra zinalazimisha mupangayi alipe kodi ya mwezi yote inayobakia. Kwa hiyo, ni lazima wewe mupangayi ukumbuke kuwa kontra ni agano. Ukiivunja mapema utapoteza pesa.</p>
<p>Note: There are conditions when a lease can be terminated without monetary penalty.</p> <ul style="list-style-type: none"> » There is domestic violence, and one or more people must leave. » The housing provider harasses the tenant or violates tenant privacy rights. » The housing becomes unsafe, uninhabitable, or violates health or safety codes. 	<p>Angalisho: Kuna wakati kontra inaweza kuvunjika bila kupoteza pesa.</p> <ul style="list-style-type: none"> » Kama kuna magonvi nyumbani, na mtu moja au zaidi wanalazimishwa kuhama. » Mwenye nyumba anasumbua mupangayi au haishimie haki ya amani ya mupangayi » Nyumba inakosa usalama, haiwezi kukaliwa ndani, au haifuate kanuni za afya na usalama
<p>Notice to Vacate</p>	<p>Tangazo ya kutoka</p>
<p>Knowing a housing provider's notice to vacate and renewal policies are essential because the lease end date determines when the notice to vacate must be given to you if the housing provider decides not to renew the lease. Or, if you, the tenant, decide to move. If the lease does have a notice to vacate clause, and notice is not given as required, your lease can be extended until the proper notification is given.</p>	<p>Ni vizuri kufahamu wakati mwenye nyumba anatoa tangazo ya kutoka na kanuni zake za kutoa kontra mupya au tarehe ya mwisho wa kontra, sababu mbele ya hiyo tarehe ni lazima akuandikie kama atakupa kontra ingine au atasimamisha ku ya kwanza. Au kama wewe mupangayi unaamua kuhama. Kama kontra ina sehemu ya kutoka lakini mwenye nyumba hakupatie tangazo ya kutoka, kontra yako itaendelea mpaka akupe tangazo.</p>
<p>Note: Even though a housing provider is not required to give a reason for a nonrenewal, a lease cannot be terminated in retaliation of any kind. Retaliation usually happens when a housing provider does not renew a lease because a tenant asserted certain rights that the provider did not want to respect. For example:</p> <ul style="list-style-type: none"> • requesting repairs • participating in a tenant group • filing a complaint with a government or other tenant support agency 	<p>Angalisho: Ijapokuwa mwenye nyumba halazimishwi kukuambia sababu ya kukataa kukupa kontra mupya, hana ruhusa ya kukatala kontra mupya sababu ya kulipiza kisasi ya aina yoyote. Mara nyingi kulipiza kisasi inatokea kama mwenye nyumba anakasirika kwa sababu mupangayi alidai haki fulani yenye mwenye nyumba hakutaka kuheshimu. Kwa mfano:</p> <ul style="list-style-type: none"> • kuomba matengenezo • kushiriki mu kikundi cha wapangayi • kupeleka malalamiko kwa serikali au kwa wasaidizi wa wapangayi



<p>EXAMPLE</p> <p>Here is the tenant’s notice to vacate process for Ms. Ineedahome. Ms. Ineedahome wants to move and decides to give her notice to vacate. Her lease requires 60 days’ notice before the end of the lease.</p> <p>Her lease ends 30 DEC 2023. To comply with the lease terms she must notify the housing provider in writing by 30 OCT 2023.</p>	<p>MFANO</p> <p>Huu ni mfano wa hatua za tangazo ya kutoka ya Bibi Ineedahome. Bibi Ineedahome anataka kuhama; anaamua kutuma tangazo yake ya kutoka. Kontra yake inamulazimisha kutuma tangazo ya kutoka siku 60 mbele ya mwisho wa kontra. Kontra yake inamalizika tarehe 30.12.2023. Kufuatana na masharti ya kontra yake, ni lazima atume barua ya kutoka kwa mwenye nyumba mbele ya tarehe 30.10.2023.</p>
--	---

<p>Subletting</p>	<p>Kukodisha Mutu Mwingine</p>
<p>This lease clause clarifies under what conditions you can sublet your unit to another tenant, and it outlines the housing provider’s screening and approval process.</p>	<p>Hii sehemu ya kontra inaeleza masharti ya mupangayi kama akitaka kukodisha nyumba kwa mutu mwingine, na inaeleza hatua mwenye nyumba atachukua kwa kuchagua na kukubali mpangayi mwingine.</p>
<p><i>NOTE: The main reason to sublet your apartment or house is that you have found a new place you want to live, but you do not want to break the lease and incur penalties.</i></p>	<p><i>TANGAZO: Sababu kubwa inayofanya mpangayi atafute mupangayi mwingine ni kama anataka kuhama ku nyumba ingine lakini hataki kuvunja kontra ya nyumba ya kwanza ili kuepuka malipo.</i></p>
<p>Modifications</p>	<p>Mabadiliko</p>
<p>This part of the lease explains the process and limits of unit changes, like adding a wall or partial wall or another structural change to a room. Modifications cannot be made without written approval.</p>	<p>Hii sehemu ya kontra inafasiria hatua na mipaka ya kubadiri nyumba, kama vile kuongeza ukuta ao nusu ya ukuta kwenye chumba, ao mabadiliko mengine katika muundo wa nyumba. Mabadiliko hayawezi kufanyika bila ruhusa yenye kuandikwa.</p>
<p>Visitor Policy</p>	<p>Kanuni ya Wageni</p>
<p>This clause states the maximum amount of time a visitor can stay in your unit. Ignoring this policy is a lease violation and can lead to eviction.</p>	<p>Hii sehemu inaeleza saa ngapi mgeni anaweza kuikala kwako. Kutofuata hii kanuni ni kuvunja kontra na inaweza kuwa sababu ya kufukuzwa.</p>
<p>Smoking Policy</p>	<p>Kanuni ya kuvuta sigareti</p>
<p>If the property has a clear no-smoking policy in the lease and there is a violation, the housing provider has a legal right to terminate the lease and begin eviction proceedings.</p>	<p>Kama nyumba ina kanuni wazi ya kukataza kuvuta sigareti, kutofuata hii sharti ni kuvunja kontra na mwenye nyumba atapata sababu ya kuanza hatua za kukufukuza.</p>

<p>Tenant Responsibilities</p>	<p>Mapashwa ya Mupangayi</p>
<p>Your obligations as a tenant are in your lease. As noted, a lease with a professional housing provider is a legally binding contract that explains all the requirements and responsibilities of renting the apartment or house you have chosen. Because it is legally binding, it is essential that a</p>	<p>Mapashwa yako ya mupangayi iko katika kontra yako. Kama ilivyosemwa mbele, makubaliano na mwenye nyumba ni kontra ya sheria unayokubali. Inafasiria masharti na mapashwa ya kukodisha vyumba ao nyumba uliyochagua. Kwa sababu inalazimisha kwa sheria,</p>

Biro ya Msaada wa Makao ya Wakimbizi ni kazi ya CWS kufuatana na makubaliano yenye inalipiwa na Wizara ya Mambo ya Nje ya Amerika.



tenant reads and fully understands a lease before signing. In addition to specific requirements written in the lease, there are common rights and responsibilities for all tenants in the U.S.	mupangayi analazimishwa kusoma na kuelewa yote yenye imeandikwa mbele ya kutia sinyatire. Zaidi ya masharti yaliyoandikwa katika kontra, kuna haki na mapashwa ya kawaida kwa wapangayi wote mu inchi ya Amerika.
Rights	Haki
The Fair Housing Act and Equal Credit Opportunity Act	Sheria ya Haki ya Nyumba na Sheria ya Usawa wa Kukopa
Because housing is a human right, you deserve the opportunity to live in a community of your choice and free from discrimination. Safe, stable, and affordable housing is not a luxury but a necessity. As a tenant, you have rights under the Fair Housing Act (FHA) and Equal Credit Opportunity Act (ECOA), as well as responsibilities to your space, housing provider, and neighbors while you occupy your unit. You must know your rights and speak out if they are being violated.	Kwa sababu fasi ya kuikala ni haki ya binadamu, unastahili kuishi katika kikundi ya batu benye unachagua na yenye haina ubaguzi. Nyumba salama, imara, na ya bei muzuri si utajiri bali ni kitu ya lazima. Kama mupangayi, una haki chini ya Sheria ya Haki ya Nyumba (FHA) na Sheria ya Usawa wa Kukopa (ECOA), pamoja na masharti kwa nafasi yako, kwa mwenye nyumba na kwa majirani unapoikala ku nyumba yako. Lazima ujue haki zako na useme kwa nguvu kama haki zako zinavunjiwa
Responsibilities	Sharti
1. Understand the Fair Housing Act and Equal Credit Opportunity Act	1. Elewa Sheria ya Haki ya Nyumba na Sheria ya Usawa wa Kukopa
2. Follow the Terms of the Lease By following the terms of your lease, you create a professional relationship with your housing provider and start building a rent payment history while meeting your tenant obligations.	2. Fuata Masharti ya kontra Kama unafuata masharti ya kontra yako, uko unajenga masikilizano ya kazi na mwenye nyumba wako na kuanza kujenga historia ya malipo ya kodi na pia unatimiza mapashwa yako ya upangayi.
3. Pay Rent on Time A key tenant responsibility is to pay the rent on time and in full. If you expect difficulty in making an upcoming payment, let your housing provider and others who are helping you know this as soon as you know it, and propose a plan to pay the rent and late fees as soon as possible. This will help avoid additional legal costs and fees.	3. Lipa Kodi kwa Wakati Sharti kubwa ya mupangayi ni kulipa kodi ya nyumba kwa wakati na yote kila mwezi. Kama unafikiri utakuwa na magumu kulipa kodi mwezi kesho, umupashe mbio mwenye nyumba na wengine wasaidizi, halafu useme wakati gani utalipa kodi pamoja na malipo ya kuchelewa. Hivi utaepuka malipo ya zaidi.
4. Keep the Apartment or House Safe and Clean It is not the housing provider's responsibility to keep the unit safe and clean — it is the tenant's. Please keep your home safe and clean.	4. Weka Chumba ao Nyumba Salama na Safi Haiko kazi ya mwenye nyumba kusafisha nyumba na kuiweka salama, ni kazi ya mupangayi. Tafazali weka nyumba yako safi na salama.
5. Do Not Damage the Apartment or House	5. Usiharibishe Chumba ao Nyumba



As a tenant, it is your responsibility to ensure that you, and any guests, do not damage your home or any other part of the premises you access, which includes common areas in apartment buildings.	Weye mupangayi ni sharti yako kuhakikisha kwamba weye na bageni bako musiharibishe nyumba yako wala eneo ingine ya kikundi kwenye munaikala.
6. Respect Neighbors with a Safe, Quiet Environment Part of being a responsible tenant is being a good neighbor. Being a good neighbor includes respecting your neighbors and refraining from behavior that disturbs their enjoyment of their home. Examples are playing music or the TV too loudly, children being too noisy or misbehaving, or arguing so that others can hear outside the apartment.	6.Heshimia Bajirani kwa makao salama na bila kelele Sehemu ya kuwa mupangayi muzuri ni kuwa jirani muzuri. Jirani muzuri ni mwenye kuheshimia bajirani bengine na mwenye kuepuka fujo yenye inaweza kuvuruga starehe katika nyumba zao. Kwa mfano kucheza muziki au television kwa sauti kubwa, au watoto wenye kufanya kelele mingi, au wenye kugombana kwa sauti ya kusikilika inje ya nyumba.
7. Make Timely Maintenance and Repair Requests Just as housing providers have clear upkeep and maintenance responsibilities, so do tenants. By reporting repair or special maintenance needs as soon as you become aware of them, you are helping the housing provider maintain the property.	7.Omba matengenezo ya bitu mbio Kama vile wenye nyumba wana masharti ya kutengeneza vitu mu nyumba, wapangayi pia biko na hiyo masharti. Kama unaomba matengenezo mbio unamusaidia mwenye nyumba kutengeneza.
<i>NOTE: If the lease or addendum does not outline how to place a maintenance order, ask the housing provider for this information before you sign your lease.</i>	<i>ANGALISHO: Kama kontra au ongezo haisemi jinsi ya kuomba matengenezo, omba mwenye nyumba akueleze mbele ya kusinye kontra</i>
8. Understand Emergency Versus Non-Emergency As a tenant, you may not face a maintenance emergency. But, if you do, it is important to know what type of maintenance is considered an emergency and what is a non-emergency. If the problem threatens health and safety or can cause injury or severe property damage, for example a roof leak or electrical outlet spark, it is an emergency. Other examples include:	8.Elewa tofauti ya jambo la hatari na yenye haiko ya hatari Mupangayi anaweza kuikala bila kuona matengenezo ya hatari. Lakini kama unaona matengenezo ya hatari, ni vizuri kujua tofauti kati ya matengenezo ya hatari na yale yasiyo ya hatari. Kama tatizo inatisha afya na usalama au inaweza kuumiza watu au kuharibu nyumba, kwa mfano paa yenye kuvuja, au moto kutokana na umeme, ni jambo la hatari. Mifano mingine ya bitu bya hatari ni kama hii :
Flooding from a clear source or from a hidden one	Mafuriko kutoka nafasi yenye kuonekana au yenye haionekani
Gas leak you can smell, regardless of the source	Harufu ya gaz kutokea mahali popote
Carbon monoxide detector alarm or smoke detector alarm going off	Kusikia kengele ya kugundua monoxyde ya carbone au kengele ya kutambua moshi
Extended power outage Bug or rodent infestations	Umeme kukatwa kwa muda mrefu. Kushambuliwa na bilulu au panya
Evidence in a toilet or sink of sewage or other water back-up	Kuona mayi ya buchafu katika choo au lavabo, au mayi ingine ya buchafu yenye kuziba



Broken furnace or heater in winter if the temperature is below 50 degrees Fahrenheit	Mashini ya joto yenye ilivunjika wakati wa baridi ikiwa hali ya joto iko chini ya 50° Fahrenheit (10° centigrade)
Broken air conditioner(s) in summer if the temperature is above 90 degrees Fahrenheit	Mashini ya baridi yenye ilivunjika wakati wa joto ikiwa hali ya baridi iko juu ya 90° Fahrenheit (32° centigrade)
Broken exterior door lock(s) that could allow intruder entrance	Mulango wa inje wenye kufuli ilivunjika inayoweza kuruhusu mwizi kuingia
It is not an emergency if the issue does not pose an immediate threat to health, safety, or property. Below are examples of maintenance non-emergencies:	Hakuna hatari kama tatizo haitishi afya, usalama, au vitu vya maana. Ifuatayo ni mifano ya matengenezo yasiyo ya hatari:
Burnt out lightbulb or broken light fixture	Ampoule au tala yenye iliharibika
Minor appliance malfunction, including the oven, microwave or one burner not working, or a broken ice maker	Kifaa chenye hakitumike vizuri kama vile jiko, microwave, au mashini ya balafu
No hot water or minor faucet leaks	Kukosa maji ya moto au bomba yenye inavuja kidogo
Noise complaints and parking disputes	Malalamiko juu ya kelele au juu ya fasi ya kuweka motokari
No heat (if the outside temperature is not below 50 degrees Fahrenheit)	Kukosa joto (kama joto ya inje iko juu ya 50° Fahrenheit—10° centigrade)
No air conditioning (if the outside temperature is not below 90 degrees Fahrenheit)	Kukosa baridi (kama baridi inje iko chini ya 90° Fahrenheit—32° centigrade)
9. Know When to Call 911 for Hospital, Fire Department, and Local Police First Responders. What is an emergency? Knowing when to call 911 instead of your housing provider might save a life and/or limit property damage. What is a 911 emergency? It is an incident, accident, or situation that is life threatening and requires immediate police, firefighter, or emergency medical personnel action. Call 911 immediately when:	9. Ujue wakati wa kupiga simu 911 kuita hospital, Zimamoto, Polisi ya karibu Matokeo ya hatari ni nini? Kujua wakati gani kupiga simu 911 kuliko mwenye nyumba inaweza kuokoa maisha ya mutu au kupunguza uharibifu wa vitu. Hatari ya 911 ni nini? Ni matokeo, ajali, au hali ya kutisha maisha na ina lazima ya polisi, Zimamoto au hatua za mbio za wafanyakazi wa waganga. Wakati wa kupiga simu 911 mbio ni huu :
FIRE You or a family member cannot put out a fire with a fire extinguisher in the apartment or elsewhere in the building.	Moto Weye au mwanafamilia wako munashindwa kuzima moto na kizimamoto chenye kiko mu nyumba au mahali pengine karibu.
INJURY Someone needs emergency medical assistance because of <ul style="list-style-type: none"> • a severe accident, especially with a head injury or major cut bleeding beyond control • having difficulty breathing and or severe chest pains • fainting/passing out or unresponsive/unconscious 	Kuumia Mutu ana lazima ya muganga haraka sababu ya <ul style="list-style-type: none"> - kuumia vibaya sana, hasa ku kichwa au kidonda inatoka damu bila kusimama - kuwa na tabu kupumua au maumivu kali ya kifua - kupoteza fahamu au kutoitika



<p>CRIME Someone sees suspicious behavior in or near your building, especially someone trying to break into your house or apartment or your neighbor's.</p>	<p>Uovu Kama unaona mutu mwenye mwenendo wa kutia shaka ndani au karibu ya jengo lako, hasa mutu anayejaribu kuvunja nyumba yako ao ya jirani yako.</p>
<p>CRIME Witness someone make a credible threat to hurt or kill someone or themselves — including in your own household.</p>	<p>Uovu Kama kuna mutu anatahisha mutu mwingine na anataka kumuua ao kujiua—hata katika nyumba yako</p>
<p>If I do not speak English well, can I call 911? Yes, 911 interpreters are available. When calling 911, know how to say in English what your language is. For example, learn and practice saying, “I speak Spanish,” “I speak Pashto,” or “I speak Arabic” in English.</p>	<p>Kama sisemi kiingereza vizuri, ninaweza kupiga simu 911? Ndiyo, watafasiri wa 911 wanapatikana. Unapoita 911, ni vizuri kujua kusema jina ya lugha yako mu kiingereza. Kwa mfano, jifunze kusema, “Ninasema Kihispania (I speak Spanish),” “Ninasema Pashto (I speak Pashto),” “Ninasema kiarabu (I speak Arabic)” katika kiingereza</p>
<p>What if I cannot hear well? How do I call 911? In most areas of the U.S., hearing and speech impaired individuals can seek assistance by texting 911. The American Disability Act requires 911 or other telephone emergency service providers to provide TTY* users with direct access to emergency services. <i>If someone in your household has these challenges, be certain to get help from your resettlement or other social service agency to understand TTY.</i></p>	<p>Halafu kama sisikii vizuri? Naweza kupiga simu 911 namuna gani? Mu sehemu mingi ya Amerika watu wasiosikia ao kusema vizuri wanaweza kupata msaada kwa kutuma SMS ku 911. Sheria ya Vilema ya Amerika inalazimisha 911 na wengine kutoa msaada kwa watu wanaotumia TTY* <i>ili wapate kupata msaada wa hali ya hatari mbio. Kama ku nyumba yako kuna mutu iko na tatizo kama hii, omba msaada kwenyi wasaidizi wako wa makao ao biro ingine ya usaidizi ili uelewe TTY.</i></p>
<p>TTY is a text telephone device for people with hearing or speech limits or disabilities. A TTY is a keyboard with a display for receiving typed text that can be attached to a telephone. The TTY user types a message that is received by another TTY at the other end of the line.</p>	<p>TTY ni simu ya kuandika na inasaidia watu wenye tatizo la kusikia ao kusema. TTY ni kama vile mashini ya kuandika. Inapokea maandishi na kuyatuma kwa njia ya simu. Mwenye kutumia TTY anaandika halafu kwa ngambo ingine mutu anapokea yale maandishi.</p>
<p>What information should I give on my 911 call? The first thing is to remain calm and be ready to answer questions and take directions from the 911 worker who answers the call.</p>	<p>Ni habari gani ninapashwa kutoa kwenye simu ya 911? Jambo la kwanza ni kuwa mtulivu na kuwa tayari kujibu maswali na kusikiliza maelekezo kutoka kwa mfanyakazi wa 911 mwenye anajibu simu.</p>
<p>Share the precise location – the exact street address and apartment floor and number – of the emergency. If you do not know the address, mention landmarks, street signs, or buildings.</p>	<p>Sema sawasawa mahali kwenye uko - anwani kamili na barabara na ghorofa na nambari – kwenye hatari. Kama haujui anwani, taja alama za mu barabara, ao majengo.</p>
<p>Know the phone number from which you are calling.</p>	<p>Ujue numero ya simu yenye unatumia</p>
<p>Give detailed information about the emergency to the dispatcher to help them determine which responder to send, i.e., medical, fire, or police.</p>	<p>Toa maelezo kamili kuhusu hatari kwa mutumayi ili kumusaidia kutuma msaidizi mwenye kufaa yaani, mganga, zimamoto ao polisi.</p>
<p>Stay on the phone with the person who answered your call – as long as being on the phone does not put you in danger.</p>	<p>Bakia ku simu na mutu mwenye alijibu simu mpaka unapooona kama kuendelea ku simu itakuletea na weye hatari.</p>



<p>Follow instructions from the person who answered the 911 call while waiting for first responders to arrive.</p>	<p>Fuata maelezo yote ya mwenye alijibu simu 911 na ungojee wale wasaidizi waliotumwa wafike</p>
<p><i>NOTE: Your housing provider cannot include a lease clause giving them the right to fine or terminate your lease because you called the police for help with an emergency.</i></p>	<p><i>ANGALISHO: Mwenye nyumba hawezi kuandika ku kontra sehemu ya kuwapa wasaidizi ruhusa ya kukutoza amande ao kuvunja kontra yako kwa sababu uliita polisi isaidie wakati wa hatari.</i></p>
<p>10. Learn About Seasonal Weatherization You can save money and energy by preparing your apartment or house for both cold winter and hot summer weather. Weatherization is protecting the exterior and interior of your apartment from weather elements to optimize energy efficiency and reduce costs. Here are some tips to weatherize your apartment:</p>	<p>10. Jifunze Mabadiliko ya Hali ya Hewa Unaweza kupunguza garama ya matumizi ya umeme, gaz na vingine kama unatayarisha nyumba yako kwa hali ya baridi na ya joto. Kujitayarisha ni kukinga nyumba ndani na inje kwa hali ya hewa ili kwa sababu ya kupunguza garama ya matumizi. Hapa tunakupa mifano ya jinsi ya kutayarisha nyumba kwa hali ya hewa:</p>
<p>SUMMER</p> <ul style="list-style-type: none"> • Hang blackout curtains on windows that are regularly exposed to direct sunlight. This blocks out sunlight so that an air conditioner can be used less. • Buy and use fans instead of air conditioning. • Close doors on unused rooms, such as bathrooms and bedrooms, during the day so the air conditioning does not reach these rooms when no one is in them. 	<p>WAKATI WA JOTO</p> <ul style="list-style-type: none"> • Weka mapasia meusi kwenye madirisha yenye inaangaziwa na jua kwa nguvu. Mapasia meusi yanazuia mwanga wa jua na inafanya mashini ya baridi isitumike mno. • Nunua na utumie ventilateur kuliko mashini ya baridi • Funga milango kwenye vyumba visivyotumika, kama vile W.C. na vyumba vya kulala, wakati wa mchana ili mashini ya baridi isitumike mu vyumba kwenye hakuna mutu
<p>WINTER</p> <ul style="list-style-type: none"> • Insulate windows by putting film on the glass panes to keep cold air from coming in. • Hang blackout curtains as thermal barriers to keep warm air from leaking outside. • Hang carpets or other fabric wall decorations on exterior walls to reduce heat loss. • Use rugs on the floors at all times as a barrier that prevents heat loss through the floor. • Use <i>draft stoppers</i> to prevent cold air from coming in under the entry door(s). <ul style="list-style-type: none"> ○ <i>NOTE: You can make a door draft stopper by rolling up a bath towel or blanket.</i> 	<p>WAKATI WA BARIDI</p> <ul style="list-style-type: none"> • Weka filamu ya plastique kwenye kioo ya madirisha ili kukinga hewa baridi isiingie. • Weka mapasia meusi kuzuia joto yenye iko ndani kuvuja nje. • Weka tapis ao mapambo ingine kwenye kuta zinaangalia inje kupunguza kupoteza joto. • Weka tapis kwenye sakafu wakati wote kuzuia joto kupotea njia ya sakafu. • Weka <i>vizuizi</i> chini ya milango ili hewa ya baridi isiingie. <ul style="list-style-type: none"> ○ <i>ANGALISHO: Unaweza kufanya kizuizi cha mlango kwa kukunja kitambaa cha kuoga ao bulangeti.</i>
<p>If you are paying for your utilities and are unable to pay your bill on time or in full, energy assistance is available. Here are some contacts for help if you are an eligible</p>	<p>Kama unalipa matumizi ya umeme na vinginevyo wewe mwenyewe na kama unashindwa kulipa kwa wakati ao kulipa yote, kuna msaada. Tazama hapo chini uone kama</p>

Biro ya Msaada wa Makao ya Wakimbizi ni kazi ya CWS kufuatana na makubaliano yenye inalipiwa na Wizara ya Mambo ya Nje ya Amerika.



<p>low-income household with high heating and cooling energy costs. You can ask about bill payment assistance, weatherization, and energy-related home repairs.</p>	<p>uko na mapato chache mwenye kustahili msaada wa kulipa. Unaweza kuomba msaada wa kulipa facture, kuinga nyumba, na kutengeneza nyumba kwa hali ya hewa.</p>
<ul style="list-style-type: none"> • LIHEAP Map State and Territory Contact Listing • A community action agency (CAA) can help with eligibility and application guidelines • NeedHelpPayingBills.com • 211 Find Help Near You 	<ul style="list-style-type: none"> • Ramani ya LIHEAP ya Mawasiliano ya Jimbo na Eneo • Biro ya Kazi ya Jamii (CAA) inaweza kusaidia kwa mambo ya kustahili na kuomba msaada • MsaadaKulipadeni.com • 211Tafuta Msaada Karibu yako
<p>11. Know Your Housing Provider’s Rights and Responsibilities</p> <p>As noted earlier, both you and your housing provider have responsibilities outlined in your lease. Because housing provider-tenant laws vary from state to state, and even from city to city, here are basic housing provider responsibilities they should follow:</p>	<p>11. Fahamu Haki na Masharti ya Mwenye Nyumba</p> <p>Kama ilivyosemwa mbele, masharti yako na ya mwenye nyumba imeandikwa ndani ya kontra yenu. Kwa sababu sheria kuhusu mwenye nyumba na mupangayi ziko mbali katika majimbo na hata katika miji, utaona hapo chini kwa kifupi masharti ya wenye nyumba:</p>
<p>FOLLOW TERMS OF LEASE AND RENTAL AGREEMENT The lease you and your housing provider sign is legally binding if it meets the state’s requirements for a valid contract, which it should. As such, the housing provider must follow all the lease terms just as you must. The links below lead to tenant rights resources and state lease requirements.</p>	<p>FUATA MASHARTI YA KUKODISHA NA MAKUBALIANO YA KUKODISHA</p> <p>Kontra yenye mulisinye weye na mwenye nyumba ni ya sheria ikiwa inalingana na sheria ya serikali ya jimbo. Kwa kawaida inapashwa kulingana nayo. Kwa hivyo, mwenye nyumba lazima afuate masharti yote ya kukodisha kama vile weye. Hapa chini kuna viungo vya kuongoza kujua haki za mupangayi na masharti ya kukodisha ya serikali ya jimbo.</p>
<ul style="list-style-type: none"> 🔗 Tenant Rights 🔗 State Laws on Leases and Rental Agreements 🔗 NOLO Landlord-Tenant Rights 	<ul style="list-style-type: none"> 🔗 Haki za Mupangayi 🔗 Sheria za Jimbo juu ya Kontra na Makubaliano 🔗 NOLO Haki za Mwenye Nyumba-Mupangayi
<p>KNOW THE FAIR HOUSING ACT (FHA) AND EQUAL CREDIT OPPORTUNITY ACT Being a housing provider is a major obligation, and understanding FHA requirements <i>plus state and local laws and housing ordinances</i> helps housing providers know their responsibilities to tenants.</p>	<p>UJUE SHERIA YA HAKI YA NYUMBA (FHA) NA SHERIA YA USAWA WA KUKOPA Kuwa mwenye nyumba ni kazi kubwa, na kuelewa masharti ya FHA pamoja na kanuni za makao za jimbo na za eneo inasaidia wenye nyumba kuelewa masharti yao kwa wapangayi.</p>
<p>WARRANTY HABITABILITY Your housing provider is responsible for providing a habitable living space. This is an apartment or house that is safe, fit to live in, free from hazards, and complies with ALL your state and local building and health codes.</p>	<p>AHADI YA UKAAJI Mwenye nyumba ana sharti ya kutayarisha nafasi inayofaa kuikala. Ni chumba ao nyumba yenye usalama, yenye inafaa kuishi ndani, bila hatari, na yenye kufuata kanuni YOTE ya jimbo na ya eneo na pia kanuni ya afya.</p>

Biro ya Msaada wa Makao ya Wakimbizi ni kazi ya CWS kufuatana na makubaliano yenye inalipiwa na Wizara ya Mambo ya Nje ya Amerika.



<p>PROVIDE RELEVANT REASONABLE ACCOMMODATION The Fair Housing Act (FHA) is a federal law that prohibits discrimination in housing. One of the many protections of the FHA is a disabled person’s right to request reasonable accommodation in rules, policies, practices, and services to allow them total access and use of the rental property. If your family has an eligible reasonable accommodation request, your housing provider must comply.</p>	<p>RUHUSU MPANGO WA MAANA NA MAFAA Sheria ya Haki ya Nyumba (FHA) ni sheria ya serikali kuu inayokataza ubaguzi katika makao. FHA ina kanuni nyingi ya kulinda watu. Kanuni mojawapo inalinda haki ya vilema ya kuomba mpango wa mafaa unayobadilisha sheria, kanuni, mazoezi, na matumizi ili kuwaruhusu vilema kuingia na kutumia makao. Kama familia yako inastahili ombi kama hii, mwenye nyumba analazimishwa kukubali kufanya mpango wa mafaa.</p>
<p>MANAGE TENANT RELATIONSHIPS WELL It is a win-win situation when you, as a tenant, have a good relationship with your housing provider. Even though the relationship is a business one, your housing provider should have a positive, helpful relationship with you.</p>	<p>Tunza Muungano wa Upangayi vizuri Wewe mupangayi ukiwa na masikilizano mazuri na mwenye nyumba, nyie bote mutapata faida. Ijapokuwa muungano ni wa kibiashara, ni vizuri kama mwenye nyumba ana masikilizano muzuri na wewe</p>
<p>MAKE TIMELY REPAIRS As stated earlier, a key housing provider responsibility is maintaining the property to be safe and habitable. Part of that is timely response to your maintenance requests. Depending on state and local laws, you may withhold partial or full rent if repairs are not done in a timely matter. If you <i>do</i> have a problem with timely maintenance, you can contact your local free legal aid agency for additional assistance.</p>	<p>FANYA MATENGENEZO HARAKA Kama ilivyosemwa mbele, sharti moja ya mweye nyumba ni Kuweka nyumba salama na inayostahili kuikala ndani. Nusu ya hivyo ni kujibu wepesi maombi yako ya matengenezo. Kuna majimbo na eneo yenye inaruhusu usilipe kodi ao kipande ya kodi kama matengenezo haifanyike kwa wakati. Kama <i>una</i> shida na matengenezo ya haraka unaweza kusema na biro ya msaada wa kisheria karibu na wewe bila malipo.</p>
<p><i>NOTE: Revisit information on pages 14-15 to review what is considered routine maintenance.</i></p>	<p><i>ANGALISHO: Tizama tena kurasa 14-15 kujikumbusha vitu gani ni matengenezo ya kawaida yaani isiyo ya hatari.</i></p>
<p>SAFETY Your housing provider’s legal responsibility and duty are to protect you in line with common sense and state and local laws that specify safety requirements for rental property. Basic safety requirements are: working smoke detectors, secure and working locks on outside doors and all windows, and lighting in dark outside areas.</p>	<p>USALAMA Sharti ya kisheria ya mwenye nyumba na mapaswa yake ni kukulinda kufuatana na akili ya kawaida na pia kufuatana na sheria zenye kutamuka masharti ya usalama wa nyumba ya kukodisha. Masharti ya msingi ni haya: vigunduzi vya moshi vyenye kutumika, kufuli kamili zenye kutumika kwenye milango ya inje na madirisha yote, na taa katika maeneo ya inje yenye giza.</p>
<p>REFUNDING SECURITY DEPOSITS IF DUE As detailed on page 11, you may qualify for a refund of your security deposit if you leave the rental</p>	<p>KURUDISHIWA MALIPO YA MWANZO KAMA INAFAA Kama ilivyofasiriwa ukurasa 11, ukiacha nyumba katika hali muzuri utarudishiwa malipo ya mwanzo kufuatana na tarehe iliyopangwa na sheria ya jimbo.</p>



property in good condition, and the deposit must be returned within state deadline requirements.	
---	--

